# Washington Poison Center

WASHINGTON
POISON CENTER
(800) 222 1222

**Nambari ya usaidizi: 1-800-222-1222**

Huduma ya bila malipo ya Washington kwa ushauri wa matibabu kuhusu sumu na utumiaji wa dawa kupita kiasi

## Dharura za sumu:

Piga simu kwa Washington Poison Center (800) 222-1222 kwa usaidizi wa matibabu katika dharura za sumu. Wataalamu wetu watakuambia ikiwa ni salama kubaki nyumbani au ikiwa unahitaji kutafuta huduma ya dharura. Ikiwa mtu hapumui, hana fahamu, au ana mtukutiko wa maungo piga simu 911.




## Ufafanuzi wa sumu:

Sumu ni kitu chochote ambacho kinaweza kuwa na madhara iwapo kitatumiwa kwa njia isiyo sahihi, kwa kiwango kisicho sahihi, au na mtu asiyefaa.

## Washington Poison Center ipo siku zote kukusaidia:

- Hufunguliwa masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki
- Wataalamu wa matibabu waliofunzwa hujibu simu zako
- Kupiga simu ni bila malipo na ni siri
- Tafsiri ya lugha inapatikana bila malipo
- Msaada wa sumu kwa watu wa kila umri
- Shirika lisilo la faida

Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya Washington Poison Center **https://www.wapc.org** au piga simu **(800) 222-1222**

## Sababu za kawaida za kupiga simu Washington Poison Center

- Ajali zinazohusiana na bidhaa za nyumbani na viwandani
- Makosa yanayohusiana na dawa
- Ufafanuzi wa sumu:
- Maswali kuhusu kutumia dawa salama
- Ushauri wa usalama kuhusu sumu

## Tunajali kuhusu afya yako pekee:

Wataalamu wetu watakuuliza kilichotokea, dutu, dalili, na historia ya matibabu husika. Pia watakuuliza jina lako na nambari ya simu kwa ajili ya kufuatiliwa baada ya matibabu. Hawatauliza kuhusu uhamiaji au hali ya kisheria.

SWAHILI

# Washington Poison Center

WASHINGTON
POISON CENTER
(800) 222 1222

**Nambari ya usaidizi: 1-800-222-1222**

Huduma ya bila malipo ya Washington kwa ushauri wa matibabu kuhusu sumu na utumiaji wa dawa kupita kiasi

## Dharura za sumu:

Piga simu kwa Washington Poison Center (800) 222-1222 kwa usaidizi wa matibabu katika dharura za sumu. Wataalamu wetu watakuambia ikiwa ni salama kubaki nyumbani au ikiwa unahitaji kutafuta huduma ya dharura. Ikiwa mtu hapumui, hana fahamu, au ana mtukutiko wa maungo piga simu 911.




## Ufafanuzi wa sumu:

Sumu ni kitu chochote ambacho kinaweza kuwa na madhara iwapo kitatumiwa kwa njia isiyo sahihi, kwa kiwango kisicho sahihi, au na mtu asiyefaa.

## Washington Poison Center ipo siku zote kukusaidia:

- Hufunguliwa masaa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki
- Wataalamu wa matibabu waliofunzwa hujibu simu zako
- Kupiga simu ni bila malipo na ni siri
- Tafsiri ya lugha inapatikana bila malipo
- Msaada wa sumu kwa watu wa kila umri
- Shirika lisilo la faida

Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti ya Washington Poison Center **https://www.wapc.org** au piga simu **(800) 222-1222**

## Sababu za kawaida za kupiga simu Washington Poison Center

- Ajali zinazohusiana na bidhaa za nyumbani na viwandani
- Makosa yanayohusiana na dawa
- Ufafanuzi wa sumu:
- Maswali kuhusu kutumia dawa salama
- Ushauri wa usalama kuhusu sumu

## Tunajali kuhusu afya yako pekee:

Wataalamu wetu watakuuliza kilichotokea, dutu, dalili, na historia ya matibabu husika. Pia watakuuliza jina lako na nambari ya simu kwa ajili ya kufuatiliwa baada ya matibabu. Hawatauliza kuhusu uhamiaji au hali ya kisheria.

SWAHILI

# Huduma ya matibabu nchini Marekani

Nchini Marekani kuna viwango tofauti vya matibabu kulingana na mahitaji yako:

**Mtoa huduma ya afya ya msingi:**
(Primary Care Doctor)

- Utunzaji wa mara kwa mara na kinga
- Muadi unahitajika
- Mifano: uchunguzi wa kimwili, hali sugu, chanjo, uchunguzi wa afya, rufaa za kitiba

**Utunzaji wa haraka:**
(Urgent Care)

- Magonjwa au hali zinazosababisha usumbufu lakini zisizo hatari kwa maisha
- Masaa hutofautiana kulingana na eneo
- Mifano: misuli iliyoteguka, mivunjiko midogo, michibuko midogo, maambukizi ya njia ya juu ya kupumua, maambukizi ya mianzi ya pua, maambukizi ya mfumo wa mkojo

**Chumba cha dharura cha hospitali**
(Hospital Emergency Room)

- Magonjwa mabaya au hali zinazohitaji huduma ya matibabu ya haraka
- Kwa kawaida hufunguliwa masaa 24 kila siku, siku saba kwa wiki
- Mifano: tatizo la kupumua, maumivu ya kifua, michibuko mikubwa, kufa ganzi upande mmoja, mitukutiko ya maungo, kukosa fahamu, ugonjwa mbaya

**Mtoa huduma wako anahitajika kutoa usaidizi wa lugha na utafsiri anapoombwa.**

**Piga simu 911** ikiwa mtu anahitaji ambulensi au mhudumu wa afya kwa hali mbaya ya kiafya.

**Piga simu 988 ikiwa mtu ana tatizo la afya ya akili.**

**Piga simu (800) 222-1222 (Washington Poison Center)** kwa dharura au maswali kuhusu kugusana na sumu.

WASHINGTON POISON CENTER (800) 222 1222


# Huduma ya matibabu nchini Marekani

Nchini Marekani kuna viwango tofauti vya matibabu kulingana na mahitaji yako:

**Mtoa huduma ya afya ya msingi:**
(Primary Care Doctor)

- Utunzaji wa mara kwa mara na kinga
- Muadi unahitajika
- Mifano: uchunguzi wa kimwili, hali sugu, chanjo, uchunguzi wa afya, rufaa za kitiba

**Utunzaji wa haraka:**
(Urgent Care)

- Magonjwa au hali zinazosababisha usumbufu lakini zisizo hatari kwa maisha
- Masaa hutofautiana kulingana na eneo
- Mifano: misuli iliyoteguka, mivunjiko midogo, michibuko midogo, maambukizi ya njia ya juu ya kupumua, maambukizi ya mianzi ya pua, maambukizi ya mfumo wa mkojo

**Chumba cha dharura cha hospitali**
(Hospital Emergency Room)

- Magonjwa mabaya au hali zinazohitaji huduma ya matibabu ya haraka
- Kwa kawaida hufunguliwa masaa 24 kila siku, siku saba kwa wiki
- Mifano: tatizo la kupumua, maumivu ya kifua, michibuko mikubwa, kufa ganzi upande mmoja, mitukutiko ya maungo, kukosa fahamu, ugonjwa mbaya

**Mtoa huduma wako anahitajika kutoa usaidizi wa lugha na utafsiri anapoombwa.**

**Piga simu 911** ikiwa mtu anahitaji ambulensi au mhudumu wa afya kwa hali mbaya ya kiafya.

**Piga simu 988 ikiwa mtu ana tatizo la afya ya akili.**

**Piga simu (800) 222-1222 (Washington Poison Center)** kwa dharura au maswali kuhusu kugusana na sumu.

WASHINGTON POISON CENTER (800) 222 1222